## Mfano wa Mpango wa Ushirika wa Kanisa

### Ushirika wa Kanisa la Ushindi *(The Victory Chapel Fellowship)*

*Jamii (Watu wote)* hualikwa kushiriki takribani kwenye shughuli zote za Kanisa la Ushindi ikiwa ni pamoja na ibada za kuabudu, mikusanyiko ya jumuiya za nyumbani, kushirikishana mahitaji, maombi, vyakula vinavyoandaliwa na usharika au kusanyiko, majadiliano yaliyoratibiwa na ushirika usio rasmi. Hata hivyo, Agano Jipya huonyesha kwamba kikundi cha watu wanaofanya kanisa la mtaa hakina budi kiwe kinachotambulika. Lazima kitambulike wazi kwa jamii kwamba ni watu gani wanaoshiriki katika kanisa hilo. Bila ya kikundi hicho kuwa kinatambulika, litakuwa ni jambo lisilowezekana kwamba kanisa lina ushuhuda mbele ya dunia, au kuweza kushirikisha ushirika wa kweli wa Kikristo ulio katika msingi wa umoja wa Ukristo usiokuwa na mipaka ya urafiki, kufanya nidhamu ya kanisa ya kibiblia, na kubeba kwa pamoja majukumu ya huduma kwa ajili ya kanisa. Kwa hiyo, majukumu kwa ajili ya huduma za Kanisa la Ushindi yanategemea kila kitu kutoka kikundi cha kusanyiko au usharika kinachoitwa "Ushirika."

### Vigezo vinavyotekelezwa na wale walioko kwenye Ushirika

Tunatambua kwamba kuna vigezo vingine maalumu ambavyo ni udhihirisho wa kukua kiroho, lakini vigezo vinavyofuata vinatoa mambo ya msingi ambayo yanaonekana kuwa ni muhimu kwa ajili ya umoja na ushirika wa kweli wa kuabudu wa Kikristo.

**(1) Maisha ya Kiroho**

Dhihirisha ushahidi wa kuokoka, matamanio ya kiroho, na msimamo kabisa wa kuenenda kwa uhusiano wa utiifu pamoja na Mungu.

**(2) Hamasa ya Kibiblia**

Epukana na uasherati, matumizi ya madawa ya kulevya, kuvuta sigara, na vinywaji vyenye kulevya.

**(3) Msimamo wa Kujikabidhi au kujitoa kabisa kwa Kanisa.**

Hudhuria ibada zote za kanisa kwa uaminifu labda uwe umezuiliwa na hali ya kiafya, kuwepo kwenye huduma nyingine, au uwepo kazini ambao hauwezi kuzuilika kwenye siku za Jumapili.

Toa sadaka yako wakati wa utoaji wa kanisa.

**(4) Umoja wa fundisho la Imani**

Umoja na uelewa wa kanuni ya imani ya Kanisa la Ushindi ni muhimu. Mchungaji huwajibika kushirikishana majadiliano ya Pamoja na muda wa maelekezo kwa kila mtarajiwa.

**(5) Maadili ya Vitendo**

Dumisha uaminifu katika aina zote za mahusiano na uaminifu katika yote uliyoamua kuwa na msimamo nayo. Dumisha tabia endelevu ya upendo na utiifu kwa wale wengine walioko kwenye ushirika.

## Sera Mbalimbali

Tunatambua kwamba baadhi ya wanachama wapya hawataendelea kuwepo, lakini tunachagua kutokuwa na kipindi cha majaribio, kwa sababu waumini wapya wanahitaji kujihusisha mara moja katika shughuli za kanisa.

Baraza la uongozi litafanya tathmini ya jina lililopendekezwa kwa ajili ya Ushirika baada ya mtarajiwa kuwa amefanyiwa usahili na mchungaji.

Mtu aliyeokoka ambaye amekubalika kuwa kwenye Ushirika atapangwa kwa ajili ya kubatizwa labda iwe kwamba alishawahi kubatizwa *(ubatizo wa maji mengi)* hapo awali baada ya kuokoka.

Endapo muumini aliyeko kwenye Ushirika ataonekana kuwa amekiuka mahitaji ya vigezo vilivyowekwa, baraza la uongozi linaweza aidha kumwondoa kwenye ushirika au kutoa muda wa kuwa chini ya uangalizi na kuwajibika, na baada ya hapo suala lake litaangaliwa au litafikiriwa tena.